

COVID-19 na Homa ya Msimu

Oktoba 2023

Homa na COVID-19 ni virusi vya kupumua vinavyoathiri mapafu na upumuaji wako. Jilinde wewe mwenyewe na wapendwa wako kwa kupata chanjo ya homa na chanjo ya nyongeza ya COVID-19.

- Chanjo ya homa huboreshwa kila mwaka ili kujikinga dhidi ya virusi au aina za homa zinazotarajiwa kuwa za kawaida au hatari zaidi.
- Dozi za nyongeza za COVID-19 zinatengenezwa ili kulinda dhidi ya aina mpya za COVID-19 ambazo zinaambukiza zaidi.
- Ni muhimu kupata chanjo yako ya homa kila mwaka na kupata chanjo ya nyongeza ya COVID-19, kila mara inapotolewa.

Kwa maelezo zaidi kuhusu chanjo ya homa tembelea bit.ly/FluPHL

Kwa maelezo zaidi kuhusu chanjo za COVID tembelea bit.ly/COVIDvaxPHL

COVID-19 na homa huenea kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa njia zinazofanana na kusababisha dalili zinazofanana, lakini husababishwa na virusi tofauti.


COVID-19 na homa zinaweza kuenezwa kupitia:



- Matone (chembe ndogo zaidi) yanaweza kukaa hewani wakati mtu aliye na COVID-19 au homa anapopumua, kupiga chafya au kukohoa, na kuruhusu virusi kumwambukiza mtu mwingine.
- Kugusa kitu au sehemu iliyo na virusi juu yake halafu kugusa mdomo, pua au macho yako.
- **Je, Wajua?** Watu walioambukizwa COVID-19 au homa huenda wasihisi dalili zozote na wanaweza kueneza virusi kwa wengine kabla wajihisi wagonjwa.

Zuia kuenea kwa COVID-19 na homa:

- Vaa barakoa ndani ya maeneo ya umma yenye watu wengi
- Nawa mikono mara nyingi
- Epuka kugusa uso wako
- Kohoa na upige chafya nyuma ya kiwiko chako au tishu



Rasilimali za COVID-19 na Homa ya Msimu

Oktoaba 2023

COVID-19 na homa huwa na dalili zinazofanana ambazo zinaweza kuanzia kwa kutokuwa na dalili hadi dalili zisizo kali au kali. Ili kupata maelezo zaidi tembelea bit.ly/FLUvsCOVID.

Vipimo vinahitajika ili kujua kama mtu ana homa, COVID-19 au pengine, zote mbili. Kupata chanjo ya homa ya msimu na chanjo ya nyongeza ya COVID-19 ndiyo njia bora zaidi ya kuendelea kulindwa.

Ili kupata chanjo na vipimo

BILA MALIPO:

Chanjo za homa
bit.ly/FluPHL

Chanjo za COVID-19
bit.ly/COVIDvaxPHL

Kupima COVID-19
bit.ly/Covid19_test

Kwa maelezo zaidi kuhusu COVID-19 na homa:

Idara ya Afya ya Umma ya Philadelphia
215-685-5488

Imefunguliwa saa za kazi za kawaida.

Piga simu kwa **711** kwa usaidizi wa TRS/TTY.

Tafsiri inapatikana,

Bonyeza **2** kwa Kihispania au ubonyeze **3** ili upate tafsiri katika lugha yako.

Tafuta huduma ya msingi ISIYOLIPISHWA au ya bei nafuu:

www.phila.gov/primary-care

Uko na bima au hauna.

Tafuta kieneo, aina ya huduma ya msingi, huduma maalum au huduma za vipimo.

Wasiliana na mtoa huduma wako wa afya ikiwa una maswali kuhusu homa ya msimu, Chanjo za COVID-19 au ikiwa unahisi mgonjwa.

Endelea Kuwasiliana Ili Upate Taarifa



Kwa maswali, tafadhali tutumie barua pepe kwa PublicHealthPreparedness@phila.gov au uache ujumbe kwa **(215) 429-3016**. Tungependa kusikia kutoka kwako!